# Mwongozo wa bajeti na changamoto kwenye sekta za viwanda, kilimo


WADAU wa masuala ya jinsia wakijadili mwongozo wa bajeti 2016/17 katika ukumbi wa TGNP Mtandao uliopo katika eneo la Mabibo jijijini Dar es Salaam hivi karibuni.

**NA SIMON NYALOBI**

HIVI KARIBUNI Wizara ya Fedha na Mipango ilitoa mwongozo wa kuandaa mpango wa bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017, ambao unaonyesha matumizi ya serikali yatakuwa sh. trilioni 22.9.

Waziri wa Fedha na Mipango Dk. Philip Mpango,alitoa mwongozo huo,kwa kuzingatia kifungu namba 21 cha sheria ya bajeti namba 11 ya mwaka 2015.

Vivyo hivyo,mwongozo wa mpango wa bajeti wa mwaka 2016/17,umejikita katika kujenga Taifa lenye uchumi wa viwanda kama ulivyoainishwa kwenye mpango wa taifa wa mwaka huu wa fedha.

Pia mpango elekezi wa miaka 15 na utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015,Malengo ya Maendeleo Endelevu(SDGS) na dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

Hivi karibuni wadau wa masuala ya kijinsia walikutana jijini Dar es Salaam,katika warsha iliyoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania(TGNP),kwa ajili ya kujadili mwongozo wa bajeti ya mwaka 2016/17 na yaliyomo katika mwongozo wa bajeti hiyo.

Ofisa Miradi wa Mtandao wa Mfuko wa Afya ya Jamii(TNCHF), Kidani Mhenga,alipata fursa ya kutoa mapendekezo kwa serikali kufikiria kupunguza mkopo wa sh. milioni 90 uliotengwa kwa ajili ya kununulia magari ya wabunge.

Kwa mujibu wa Kidani,wabunge wangepewa mkopo wa sh.milioni 20 na sh. milioni 70 zingetumika katika shughuli za maendeleo za jimbo la mbunge.

"Wafikirie kupunguza matumizi yasiyo ya lazima kumpa mbunge mkopo wa kununulia gari kwa kusema kweli tunakuwa hawatutendei haki wananchi, hili waliangalie upya," anasema.

Kidani anashauri fedha bajeti ya ujenzi wa miundombinu ilekezwe zaidi katika barabara za vijijini ili mazao ya chakula na biashara,yaweze kusafirishwa kwa urahisi akilinganisha na hali ya sasa ambapo usafiri ni mgumu.

Ofisa miradi huyo wa TNCHF anafafanua kwa kufanya hivyo bajeti hiyo itaweza kuwagusa moja kwa moja kwa wakulima hususan wakulima wadogo katika jitihada zao za kujikwamua katika dimbwi la umasikini.

Kuhusu pembejeo za kilimo kwa wakulima wadogo,anashauri serikali ifikirie katika bajeti kuweka utaratibu wa kupeleka matrekta kila tarafa,kata na kila kijiji ili kurahisisha shuhuli za kilimo.

Kidani anatahadharisha kuwa iwapo wakulima wadogo hawatawezeshwa kupata matrekta ya kulimia hawataweza kuzalisha mazao ya kutosha na hatimaye kusababisha kuwepo na njaa nchini.

Anaeleza hali hiyo ya itaathiri utendaji wa wafanyakazi wa maeneo ya mjini kwani hawataweza kuongeza ufanisi wa kazi zao kutokana na kuhangaikia chakula cha familia zao.

Akizungumzia suala la uanzishwaji wa viwanda, Kidani anaipongeza serikali ya awamu ya tano chini ya Rais Dk. John Magufuli kwa kuja na mpango huo kwani utasaidia kuongeza ajira na pia masoko ya mazao ya wakulima.

Hata hivyo,anaiangukia serikali kutilia mkazo viwanda vidogo ambavyo anaeleza vitasaidia kuongeza thamani ya mazao yao wanayolima badala ya kuyauza yakiwa ghafi.

"Viwanda vidogo vitasaidia wakulima kwa mfano kule Muheza Tanga,vijengwe viwanda vidogo kwa ajili ya machungwa na mkoa wa Dodoma viwanda vya zabibu kule kuna zabibu nyingi," anasisitiza.

Kidani anashauri kasi ya uchimbaji wa visima vya kudumu katika maeneo ya vijijini itiliwe mkazo,uende pamoja na mipango ya utandazaji wa mabomba ya maji katika maeneo ya mjini.

Kwa mtazamo wake,visima vikiwa vingi maeneo vijijini vitawapunguzia adha wanawake ya kutembea muda mrefu kutafuta maji na badala yake watajikita katika shughuli za kilimo.

Anafafanua wanawake wanaoishi katika maeneo ya mijini ndiyo wanaoshiriki katika shughuli za kilimo kwa asilimia kubwa,hivyo wakisaidiwa katika upatikanaji wa maji wataweza kuzalisha mazao maradufu ikilinganishwa na sasa.

Kwa upande wake,Mkurugenzi wa Shirika lisilo la serikali linaloshughulikia masuala ya Kilimo Mkoa wa Mbeya(MIICO),Adam Siwingwa, anahofia mkazo wa uanzishwaji wa viwanda vingi na uhusiano wa sekta ya kilimo.

Siwingwa,anashauri serikali kutoa ufafanuzi kuhusu uhusiano kati ya sekta ya viwanda na kilimo ili kuwapa maarifa wakulima ambao kwa sasa wanafikiria kuwa wametengwa na serikali ya awamu ya tano.

"Hiki kipaumbele cha viwanda kimeonekana kama kinahatarisha kilimo,wapo watu sasa hivi wanafikiria kuacha kilimo waende kufanya kwenye viwanda kama serikali inavyosisitiza," anaeleza.

Kwa mujibu wa Siwingwa,serikali ionyeshe moja kwa moja katika bajeti kilimo ni eneo wezeshi la viwanda,zaidi ya kuonyeshwa kuwa kitapewa kipaumbele kusaidiwa.

Siwingwa anasisitiza kilimo kipewe rasilimali fedha na watu kwani bila ya chenyewe mustakabali wa kuwa na viwanda vyenye ufanisi itakuwa ndoto isiyotimizwa.

Akizungumzia mgawanyo wa bajeti wa shughuli za kawaida na maendeleo,ambayo ni asilimia 73 kwa shughuli za kawaida na asilimia 27 ya maendeleo,anasema mgawanyo huo si sahihi.

Anashauri mgawanyo huo ubadilishwe kwani bila ya kuweka bajeti kubwa katika shughuli za maendeleo,malengo ya serikali yanaweza kutofikiwa kwa kasi inayotakiwa na serikali.

Hata hivyo,anaikumbusha serikali kuzingatia Mkataba wa kimataifa wa Maputo uliosainiwa mwaka 2003,ambao ulizitaka nchi kutenga asilimia 10 ya bajeti katika bajeti za serikali duniani.

Katibu Mtendaji wa Chama Cha Wazalishaji wa Korosho(LUKWIKA) cha mkoani Mtwara, Hassan Namagono,anafarijika msisitizo uliowekwa katika uanzishwaji viwanda katika mwongozo wa bajeti kwa kuwa wakulima wa zao la korosho watanufaika.

Anasema kutokana na ujio wa viwanda vingi vya korosho vitasaidia ubanguaji wa korosho kufanyika mkoani Mtwara bila ya kusafirishwa zikiwa ghafi.

"Kipato cha mkulima kitaongezeka, kwa mfano leo hii mkulima anauza korosho yake ikiwa ghafi kwa kilo sh. 1,000,lakini kama itabanguliwa kilo hiyo hiyo moja atauza kwa sh. 5,000 hadi 6,000," anasema.

Akizungumzia udhibiti wa mfumuko wa bei unaotarajiwa kufanywa na serikali,Namagono anasema serikali inatakiwa kufafanua njia za kudhibiti ili wananchi waweze kuelewa kwani kwa sasa walivyoweka katika mwongozo wa bajeti 2016/17 haujaeleza kinaganaga.

Vilevile Mratibu wa Kituo cha Taarifa na Maarifa(TIGUSHE) cha mkoani Mbeya,Flora Mathias,anaipongeza serikali kuelekeza katika bajeti yake samani za wazawa kutumika katika ofisi za serikali na kupiga marufuku samani za nje.

Flora anaeleza hatua ya kupiga marufuku ununuzi wa samani za nje katika matumizi ya serikali utawasaidia watengenezaji wazawa kufaidika na kuboresha biashara zao.

Akizungumzia viwanda,anasema serikali inatakiwa kuhakikisha viwanda vinavyoanzishwa katika mkoa husika viendane na aina ya mazao yanayolimwa kwa wingi.

Kuhusu ongezeko la ajira litokanalo na uanzishwaji wa viwanda,Flora anashauri katika bajeti idadi ya ajira zinazotarajiwa kuzalishwa zianishwe ili ifahamike kila mwaka zinazalishwa ajira ngapi tofauti na sasa ambazo zimeelezwa kwa ujumla.

Naye mwanafunzi wa Stashahada ya sheria katika chuo cha Royal,kilichopo jijini Dar es Salaam, Datus Inshasha,anaiasa serikali kuangalia upunguzaji wa bei ya zana za kilimo ili kumnufaisha mkulima wa kawaida.

Hata hivyo,Inshasha anaishauri serikali kuweka utaratibu wa kulazimisha wafanyabiashara wa zana za kilimo kuweka maduka yao,katika maeneo ya kilimo badala ya maeneo ya mjini ambako wakulima hupata shida kuzifuata.

